

**RAISI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA DKT
JOHN POMBE MAGUFULI AMTEUA NDUGU HASSAN ABEID
MWANG'OMBE KUWA POSTAMASTA MKUU WA SHIRIKA LA POSTA
TANZANIA.**



***Ndugu Hassan Mwang'ombe, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta
Tanzania.***

Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kupitia barua yake iliyotolewa tarehe 19 Machi 2019, amemteua Ndugu Hassan Abeid Mwang'ombe kuwa Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania. Uteuzi huo umeanza rasmi tarehe 12 Machi 2019.

Kabla ya kuteuliwa rasmi kushika nafasi ya Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Ndugu Mwang'ombe alikua akikaimu nafasi hiyo. Pia aliwahi kuhudumu katika nafasi mbalimbali kwenye Shirika la Posta ikiwemo Meneja mkoa katika mikoa ya Mbeya, Shinyanga na Dar es salaam. Na aliwahi kushika nafasi ya Meneja Mkuu uendeshaji biashara wa Shirika la Posta Tanzania.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-22-2114512, 2116898
Barua pepe: press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz
Nukushii: 255-22-2113425



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA BARACK OBAMA,
11400 DAR ES SALAAM,
Tanzania.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ikulu, Dar es Salaam.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli amemteua Bw. Hassan Abeid Mwang'ombe kuwa PostaMasta Mkuu.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi John Kijazi imeeleza kuwa uteuzi wa Bw. Mwang'ombe umeanza tarehe 12 Machi, 2019.

Kabla ya uteuzi huo, Bw. Mwang'ombe alikuwa akikaimu nafasi hiyo.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Gerson Msigwa'.

Gerson Msigwa
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, IKULU
Dar es Salaam
19 Machi, 2019

***Barua ya uteuzi wa Ndugu Hassan Abeid Mwang'ombe kuwa
Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania.***